

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
15 Novemba 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Elia Kimena
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
George Kabogo
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Ayuba
Kibwana Mohammad Msiga
Mohammed Samwely
Mussa Alex
Paulo Atibu Hatibu
Shamte J Kigoma

Msafara wa Baisikeli

Elaine ameandaa photocopy za risiti zote lakini bado hajaprint picha za msafara kwa ajili ya repoti kwenda kwa wadhamini wa msafara.

Mawasiliano na serekali

Elaine alitembelea serekali la jiji kuuliza kuhusu idara gani inahusika na mambo ya baisikeli sasa baada ya idara ya DART ya Mama Mlambo kuwa agency yenye uhuru. Aliongea na Mama Msonde na Neema Kinyago ambao walimwambia kuna idara inayoitwa “Mipango ya miji, mazingira na usafirishaji” na kiongozi ni Martha Mkupasi. Elaine alisema atawasiliana nao kutayarisha mkutano na Mama Mkupasi na wanachama wa UWABA.

Kwa bahati pia Elaine alikutana na Ulrich Malisius ambaye anafanya kazi ya mipango ya jiji na yupo ofisi ya “Urban Authorities Support Unit” ya “Prime Minister’s Office Regional Administration and Local Government”, na anapenda sana kuhamasisha usafiri wa baisikeli.

Dieter Schelling wa Benki ya Dunia alitualika kwenye mkutano ofisi ya DART, Ubungo alhamisi saa nane mchana kuhusu njia za baisikeli. Alipendelea watu wawili wahudhuri basi Elaine na Mejah watahudhuria.

Mradi wa Wamba

Kuna nafasi ya walimu sita kwenye kozi ya usalama wa baisikeli shule ya Msongole. Wanachama kumi walipenda kufundisha basi kila mtu alisimama kueleza kwa nini yeye atakuwa mwalimu mzuri na tulifanya uchaguzi. Filbert Mbecha, Frank Peter, Hamadi Bwaja, Bashiri Rashidi walichaguliwa kwanza na baada ya hapo Edgar Paulo na Hussein Hamza walichaguliwa.

Elaine aliandaa fomu za maswali na tulipitia na kurekebisha. Pia aliprint mwongozo, karatasi za mahudhurio na atatayarisha cheti.

Elaine na Juma walichukua Tsh 910,000 kutoka benki na tuliweka hela hii pamoja na Tsh 144,000 ya hela ya UWABA ambayo Elaine anayo na Tsh 60,000 ya hela ya UWABA ambayo Juma anayo iwe Tsh 1,114,000.

Mejah alitumia Tsh 480,000 kununua helmeti ambazo amepeleka ofisini. Juma alitumia Tsh 300,000 kununua jaketi za reflecta 60. Tsh 84,000 ilichukuliwa na Filbert kama badjeti ya bites kwa wanafunzi wote kila siku. Tsh 10,000 ilichukuliwa na Hamadi and Filbert kusafirisha helmet na jaketi. Filbert na Hamadi pia walichukua Tsh 60,000 kwa posho yao ya chakula na makazi. Edgar alichukua Tsh 72,000 kama badjeti ya photocopy ya mwongozo, karatasi za mahudhurio, cheti na maswali. Bashiri alichukua Tsh 120,000 kama posho yake pamoja na ya Frank, Edgar na Hussein.

Tulikuwa na wasi wasi kwamba kutakuwa na mgoma wa waalimu na vipi itaziba mafunzo yetu. Elaine alimpigia simu mwalimu mkuu wa shule ya Mbondole na alisema kwamba wanafunzi watakuwepo na mafunzo yataendelea.

Filbert na Hamadi watasafiri kwenye basi jumapili na helmet na vifaa vingine na wengine watasafiri Jumatatu na baisikeli na mafunzo yataanza jumanne.

Mashindano ya wimbo

Mwanachama mpya Elia ameandaa wimbo ya hip hop kuhusu baisikeli. Aliimba na wanachama walipenda sana. Tuliamua baada ya mafunzo ya Msongole tutafuatalia kupata mdhamini wa mashindano ya wimbo.

Mambo ya hela

Juma anabaki na Tsh 2,500 ya hela ya UWABA. Ally Saidi Mwishehe hajaleta hela ya guta kwa wiki nne.